

Boga linalobingirika

- Hadithi kutoka Iran

Det rullende gresskaret

- En fortelling fra Iran

Hapo zamani za kale, mwanamke mzee sana (ajuza) alikuwa anaishi kwenye kijiji kidogo kilichokuwepo pemberi ya msitu hatari nchini Irani. Alikuwa na mtoto wa kike (binti) aliyeolewa na kuishi upande wa pili wa msitu. Alimkumbuka sana, mtoto wake wa kike na akaamua kufunga safari kwenda kumtembelea wakati wa sikukuu ya Eid.

Det var en gang en gammel dame som bodde i en liten landsby ved siden av en stor og farlig skog i Iran. Hun hadde en datter som var gift og bodde på den andre siden av skogen. Hun savnet datteren sin og en dag bestemte hun seg for å dra og besøke henne til Eid.



Ili aweze kufika upande wa pili inambidi (ni lazima) akatize kwenye msitu ule hatari. Akajiandalia chakula, akavaa viatu na gauni lake jeusi refu lenye maua maua na kuondoka. Mwanamke mzee sana (Ajuza) alikwenda na kwenda, mpaka akapotelea ndani ya msitu.

Wakati akiwa anakwenda akawa animba:

(Mpendwa mtoto wangu wa kike mimi nakupenda, umeondoka na kuelekea sehemu ya ajabu na mimi natamani kukuona wewe.)

For å komme dit, måtte hun krysse den farlige skogen. Hun gjorde i stand en skreppe med mat, tok på seg sko og sin lange svarte blomstrede chador, og dro av sted. Hun gikk og gikk, helt til hun forsvant dypt inni skogen. Mens hun gikk sang hun:

Alå doxtar balå qorbunatam man, be ghorbat rafti o heirunatam man.

(Min kjære datter jeg elsker deg, du har dratt til et fremmed sted og jeg leng-ter etter deg.)



Ghafla akawa ametokea mbwa mwitu (wa msituni) mbele ya ajuza, ajuza alistuka.

(Nam,nam,nam, kwa chakula kitamu sana) alisema mbwa mwitu huku akizunguka kwa kutamani sana

Ajuza akajiweka sawa na kusema: "mimi si chakula kitamu sana, mimi ni mwembamba na tumbo tambarare. Mwili wangu una mafuta kiasi, ukinila mimi hautashiba" Mbwa mwitu (wa msituni) mdomo wake ukakauka na kusema

"Nifanye nini sasa, mimi nina njaa?" Ajuza akajibu: "niache niende kwa mtoto wangu wa kike kwenye sikukuu ya Eid na nitakula wali (mchele uliopikwa) kwa nyama ya kondoo. Nitakapokuwa nimeshiba na mnene, nitakuja na utanila mara moja"

Mbwa mwitu (wa msituni) alifikiria hilo ni wazo zuri sana na akamuamuru ajuza afanye haraka, kabla yeye hajawa na njaa kali sana.

Ajuza akaondoka kwa haraka.

Plutselig var det en ulv som dukket opp foran den gamle damen, og hun stivnet til.

«Nam, nam, nam, for et deilig måltid,» sa ulven og siklet grådig.

Den gamle damen tok seg sammen og sa: «Jeg er da ikke deilig mat, jeg er tynn med mage flat. Kroppen min har lite fett, spiser du meg, blir du ikke mett.»

Ulven ble helt tørr i munnen og sa: «Hva skal jeg gjøre da, jeg er så sulten?»

Og gamle damen svarte: «La meg dra til min datter til Eid og spise ris med lammespyd. Når jeg har blitt tjukk og mett, kommer jeg som en deilig rett, som kan spises på ett brett.»

Det syntes ulven var en god idé og han ba den gamle dama om å skynde seg, for han var kjempesulten! Hun skyndte seg av gårde.



Ghafla akatokea **tiger** (mnyama mkubwa aina ya paka mwenye mistari) akitokea juu ya mti. Yule tiger alionesha makucha yake makali na kusema: (Nam, nam, nam, kwa chakula kilicho kitamu!)

Ajuza akajibu tena: "mimi si chakula kitamu sana, mimi ni mwembamba na tumbo tambarare. Mwili wangu una mafuta kiasi, ukinila mimi hautashiba" Kisha kucha za **tiger** zikarudi kwenye miguu yake na alisema:

"Nifanye nini sasa? Mimi nina njaa!" Ajuza akajibu tena:

"niache niende kwa mtoto wangu wa kike yangu kwenye sikukuu ya Eid na nitakula wali (mchele uliopikwa) kwa nyama ya kondoo.

Nitakapokuwa nimeshiba na mnene, nitakuja na utanila mara moja."

Tiger akakubali na kumuomba aharakishe kurudi, kwa sababu yeye alikuwa na njaa kali sana. Yule ajuza akaondoka kwa haraka eneo lile.

Plutselig kom det en tiger og hoppet ned fra et tre foran henne. Tigeren viste fram de skarpe klørne sine og sa: «*Nam, nam, nam, for et deilig måltid!*». Igjen svarte gamle dama: «*Jeg er da ikke deilig mat, jeg er tynn med mage flat. Kroppen min har lite fett. Spiser du meg, blir du ikke mett.*»

Da forsvant tigerens klør inn i potene og han sa: «*Hva skal jeg gjøre da? Jeg er så sulten!*»

Igjen, svarte gamle dama: «*La meg dra til min datter til Eid, og spise ris med lammespyd. Når jeg har blitt tjukk og mett, kommer jeg som en deilig rett, som kan spises på ett brett.*»

Tigeren gikk med på det og ba henne skynde seg tilbake, fordi han var veldig sulten. Den gamle konen skyndte seg av sted.



Ghafla akatokea simba akinguruma mbele ya uso wa ajuza huku nywele zake zikiwa zimemtapaka shingoni.

“Ngoja! Ni heshima kwangu kuliwa na simba - mfalme wa msitu! Lakini mfalme anastahili chakula bora” alisema yule ajuza na kuendelea:

“Mimi si chakula kitamu sana, mimi ni mwembamba na tumbo tambarare. Mwili wangu una mafuta kiasi, ukinila mimi hautashiba”

Simba alivyosikia hivyo, nywele zikamshuka kwa kulala chini ya kichwa chake na kusema: “Nifanye nini sasa? Mimi sijala kwa muda wa wiki (juma) moja sasa!” Kama kawaida akajibu ajuza: “Niache niende kwa mtoto wangu wa kike kwenye sikukuu ya Eid na nitakula wali (mchele uliopikwa) kwa nyama ya kondoo. Nitakapokuwa nimeshiba na mnene, nitakuja na utanila mara moja.”

Simba aliwaza hilo ni wazo zuri, aka ahidi kumsubiria hadi atakaporudi ajuza.

Plutselig var det en løve som stod og brølte rett i ansiktet på den gamle dama, mens manken hans strittet til alle kanter.

«Vent! Det er en ære for meg å bli spist av løven - skogens konge! Men kongen fortjener da et bedre måltid,» sa den gamle dama og fortsatte: «Jeg er da ikke deilig mat, jeg er tynn med mage flat. Kroppen min har lite fett, spiser du meg, blir du ikke mett.»

Da løven hørte dette, falt manken slapt rundt hodet hans og han sa:

«Hva skal jeg gjøre? Jeg har ikke spist på en uke!»

Som vanlig svarte gamle dama: «Jeg er da ikke deilig mat, jeg er tynn med mage flat. Kroppen min har lite fett. Spiser du meg, blir du ikke mett.» Og løven, som syntes dette var en god idé, lovte å vente til hun var tilbake.



Giza lilipofika, ikawa mwanamke mzee sana (ajuza) mwishowe amefika nyumbani kwa mtoto wake wa kike. Alikuwa na furaha sana kumuona mtoto wake wa kike na hata kusahau yote yaliyotokea njiani. Alikaa kwa mtoto wake kwa siku saba na alikula chakula kingi sana kizuri.

Ikaja siku ya kuaga aweze kuondoka. Ghafla akakumbuka wanyama wote wakali wanao mngojea njiani kumla, akamuelezea mtoto wake wa kike juu ya hilo. Wakakaa chini na kuanza kufikiria.

Da det hadde blitt mørk, kom den gamle dama endelig fram til datteren sitt hus. Hun ble så glad av å se datteren sin at hun glemte alt som hadde skjedd på veien. Hun ble hos sin datter i syv dager og syv netter og spiste masse god mat. Så kom dagen da hun skulle ta farvel. Plutselig husket hun alle de farlige dyrne som ventet på henne langs veien og ville spise henne, og fortalte dattera si om dette. De satt seg ned og begynte å tenke.



Ghafla wakapata wazo. Wakaenda sokoni na kununua boga kubwa sana na kurudi nalo nyumbani. Wakachukua nyenzo (vifaa) mbalimbali kama kijiko, uma, sululu na koleo (chepe, beleshi). Kwanza walianza kwa kukatengeneza mfuniko wa boga. Walipomaliza waka likwangua na kulichimba boga sehemu ya ndani. Walichimba, walichimba, walichimba na kuhakikisha wameondoa sehemu yote ya ndani ya boga. Pakawa nafasi kubwa ndani ya boga

Plutselig fikk den idé: De dro til basaren og kjøpte et stort gresskar og tok det med seg hjem. De skar ut et lokk ut av toppen. Også tok de fram skje, gaffel, hakke og spade, og gravde ut innholdet. De gravde og gravde og gravde, helt til det ble et tomrom inni gresskaret. Så tok den gamle damen skreppen sin og hoppet inni gresskaret.



Ajuza akachukua kifurushi chake na kuingia ndani ya boga. Mtoto wake wa kike akaweka mfuniko. Mtoto wake wa kike, mume wake pamoja na wana kijiji wengine wakali lisukumiza boga.

Datteren la på lokket. Sammen med mannen sin og de andre i landsbyen rullet de gresskaret av sted
Gresskaret rullet og rullet og rullet og forsvant dypt inni skogen.



Boga lika bingirika na kubingirika na kupotela ndani ya msitu. Ghafla kichwa cha ajuza kikajigonga kwenye kuta za boga.

Alikuwa ni simba amelisimamisha boga kwa mguu wake. Simba akaliuliza boga huku akiliangalia:

“Boga linalobingirika, niambie: Umemuona mwanamke mnene wakati ukipita njiani?”

“Hapana, nibiringishe, nibiringishe kutoka hapa” alijibu ajuza akiwa ndani ya boga. Simba akalipiga teke na kulibingirisha boga kutoka sehemu ile.

Plutselig traff hodet til den gamle dama gresskarveggen. Det var løven som hadde stanset gresskaret med den ene foten sin. Løven så på gresskaret og spurte:

«*Rullende gresskar, fortell meg: Har du sett en fet dame på din vei?*»

«*Nei walla, rull meg, trill meg, herifra,*» svarte den gamle damen inni gresskaret.

Og løven sparket og rullet gresskaret fort av sted.



(Dunk!) safari hii alikuwa **tiger** alie lisimamisha boga. **Tiger** akauliza:

“Boga linalobingirika, niambie: Umemuona mwanamke mnene wakati ukipita njiani?”

“Hapana, nibiringishe, nibiringishe kutoka hapa” **tiger** alisikia boga likisema, hivyo akalibiringirisha boga toka sehemu ile.

«Dunk!» Denne gangen var det tigeren som hadde stoppet gresskaret. Tigeren spurte:

«Rullende gresskar, fortell meg: Har du sett en fet dame på din vei?»

«Nei walla, rull meg, trill meg, herifra,» hørte han gresskaret si, så han rullet gresskaret av sted.



(Dunk!) Tena kichwa cha ajuza kikajigonga kwenye kuta za boga. Safari hii alikuwa mbwa mwitu (wa msituni) alie lisimamisha boga kwa kutumia sehemu ya mbele ya pua yake. Mbwa mwitu (wa msituni) akanusa boga na kuuliza:

“Boga linalobingirika, niambie: Umemuona mwanamke mnene wakati ukipita njiani?”

“Hapana, nibiringishe, nibiringishe kutoka hapa” boga lilisema.

«Dunk!» Igjen traff hodet til gamle dama gresskarveggen. Nå var det ulven som hadde stanset gresskaret med snuten sin.

Ulven sniffet på gresskaret og spurte: «Rullende gresskar, fortell meg: Har du sett en fet dame på din vei?»

«Nei walla, rull meg, trill meg, herifra,» sa gresskaret.

Men ulven kjente igjen stemmen til den gamle dama. Med de skarpe tennene sine tok han opp lokket og hopt inni gresskaret. Men den gamle dama hadde laget et lokk på den andre siden av gresskaret også. Hun åpnet lokket og hoppet ut fra denne siden. Hun var rask og la lokket tilbake. Dermed fikk ulven lokket midt på snuten. Så skyndte hun seg til toppen av gresskaret og la på det lokket også. Nå var ulven innestengt i gresskaret.



Lakini mbwa mwitu (wa msituni) alitambua sauti ya yule ajuza. Kwa kutumia meno yake makali akafanikiwa kufungua mfuniko na kuingia ndani ya boga. Lakini ajuza alikuwa ametengeneza mfuniko sehemu ya pili ndani ya boga pia. Alifungua mfuniko na akaruka nje kutokea upande huo kwa haraka. Mbwa mwitu (wa msituni) alijaribu kumkamata hakufanikiwa akawa amefunikwa na mfuniko katikati ya pua yake. Ajuza kwa haraka akapanda mpaka juu ya boga na kuweka mfuniko mwengine. Mbwa mwitu (wa msituni) akawa amefungiwa ndani ya boga.

Yule ajuza, aliyekula chakula chenye mafuta na kupata nguvu, akakusanya nguvu zake zote na kusukumiza boga toka mahali pale, likiwa na mbwa mwitu ndani.

Boga lilibingirika na kubingirika, na mwishowe kuanguka chini katika bonde lenye giza nene.


Ajuza akiwa ameridhika na mwenye furaha aliondoka kuelekea nyumbani. Alipofika nyumbani alijitengenezea chai kwa ajili yake.

Na huo ndio mwisho wa hadithi.

Den gamle dama, som hadde spist seg fet og sterke, samlet alle sine krefter og trillet gresskaret av sted, med ulven inni. Gresskaret rullet og rullet, og falt til slutt ned i en dyp, mørk dal. Fornøyd og glad dro den gamle damen hjem og lagde litt te til seg selv.

Snipp snapp snute, så var eventyret ute.





Illustratør: Svetlana Voronkova

Se flere fortellinger på morsmal.no